

# Nalilia nchi yangu

Moyoni nakulilia, yatokeayo vituko,  
Moyoni sijatulia, nimepata mushituko,  
Ukabila wazi pia, umoja kwetu maziko,  
Oh Kenya yangu jamani, moyoni nakulilia.

Siasa meshika kazi, kila mtu jitetea,  
Mekaribia chaguzi, amani tunaombea,  
Twahimiza viongozi, wananchi sijechochea,  
Oh Kenya yangu jamani, moyoni nakulilia.

Sera ziwe nguzo yetu, kabila tuweke mbali,  
Tushirikiane kwetu, vyama tusije kujali,  
Matendo yawe ya utu, tusaidiane hali,  
Oh Kenya yangu jamani, moyoni nakulilia.

Ukabila tukatae, tupendaneni pamoja,  
Undugu kwetu tukae, tujenge wetu umoja,  
Shirikiano tutwae, tuvumiliane waja,  
Oh Kenya yangu jamani, moyoni nakulilia.

JOSPHAT CHERUIYOT,